

**TAARIFA YA MRADI WA SHAMBA LA MITI LA FAMILIA YA  
WULSTAN MHAGAMA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA  
UHURU KITAIFA NDUGU, CHARLES FRANCIS KABEHO TAREHE**

**05-06-2018**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018**, Tunayo furaha kubwa kukuaribisha wewe pamoja na msafara wote uliofuatana nao hapa katika hifadhi ya mazingira Kijiji cha Kilimani nasema karibu sana.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018**, Mradi huu wa hifadhi ya Mazingira (shamba la miti), ulianzishwa mwaka 2012 ikiwa na idadi ya miti 4900 aina ya Misindano (pinus patula) ambalo lina ukubwa wa ekari 7.

**Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018**, Shamba hili ni kielelezo cha mashamba yote yenye ukubwa wa ekari 3570 yenye jumla ya Miti 1,785,000 .

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018**, Gharama iliyotumika kwa shughuli za uanzishwaji na utunzaji wa shamba hili hadi kufikia sasa ni jumla ya kiasi cha Tshs 7,000,000/=

**Ndugu kiongozi wa mbio za mwenge kitaifa 2018**, Lengo la mradi huu ni kutekeleza Sera ya Mazingira ya kuwa na hifadhi endelevu ya mazingira na kuongeza kipato cha familia ili kumudu gharama za maisha ikiwemo kusomesha pamoja na uhifadhi wa mazingira utakaowezesha Wanafunzi kupata elimu juu ya uhifadhi wa mazingira.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018**, Tunaamini ya kwamba ili kuwe na utunzaji endelevu wa rasilimali misitu na uoto wa asili pamoja na utunzaji wa vyanzo vya maji kunahitajika kuwa na Jamii iliyoelimika hivyo sisi kama familia tunaunga mkono kauli mbiu inayosema **“Elimu ni Ufungua wa Maisha, Wekeza sasa kwa Maendeleo ya Taifa letu”**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018**, Baada ya taarifa hii, kwa heshima na taadhima nakuomba ukague shamba hili familia ya Ndugu Wulstan Mhagama.

Ni mimi,

**JOSEPHINE GILLO  
Kny:MKURUGENZI WA MJI  
HALMASHAURI YA MJI  
MBINGA**